TANGAZO LA SERIKALI Na. 356 la tarehe 4/7/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 155)*

SHERIA NDOGO ZA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA ZA MWAKA 2025

Jina

**1**. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa Mwaka 2025.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hizi zitatumika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa .

Fasili

**3**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

"machinjio" maana yake ni sehemu inayomilikiwa na mtu au taasisi iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"mazao ya mifugo" maana yake ni nyama, ngozi, pembe, samadi, maziwa na vitu vingine vitokanavyo na mifugo;

"meneja wa machinjio" maana yake ni mtu aliyeteuliwa au kuajiriwa na Halmashauri kusimamia shughuli za machinjio;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, mbwa, paka, kuku na inajumuisha ndege na wanyama wengine wanaofugwa na binadamu;

"mkaguzi wa nyama" maana yake ni mtaalam wa afya ya mifugo aliyeajiriwa na Serikali na kusajiliwa au kuorodheshwa au kuandikishwa na Baraza la Veterinari Tanzania;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki wa machinjio" maana yake ni mtu au taasisi inayomiliki machinjio katika eneo la Halmashauri;

"operesheni" maana yake ni mpango maalum uliondaliwa na Halmashauri unaohusisha maafisa wa Halmashauri, wataalam mbalimbali na wadau kutoka vyombo vya usalama kwa ajili ya ukaguzi, ukamataji na uzuiaji wa makosa yatokanayo na migogoro ya ufugaji usiozingatia matwaka ya Sheria Ndogo hizi;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji na ulishaji wa mifugo ndani ya jengo, zizi au eneo lenye uzio lililoruhusiwa na Halmasahuri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi; na

"zurura" maana yake ni kitendo cha mfugo kuwepo eneo lisiloruhusiwa kwa mujibu wa mpango wa matumizi bora ya ardhi au kwa kuzingatia makubaliano ya mkutano mkuu wa kijiji.

Kazi za Halmashauri

**4**. Halmashauri itakuwa na kazi za-
(a) kusimamia maandalizi na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi;
(b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji anaruhusiwa kufuga kulingana na ukubwa wa eneo lake;

(c) kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii ili kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kutoa chanjo kwa kushirikiana na wafugaji ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza binadamu;
(g) kudhibiti uzururaji wa mifugo na wanyama katika Halmashauri kwa mujibu wa Sheria;
(h) kutenga maeneo maalum ambayo ni njia maalum kwa ajili ya kupitisha mifugo kutoka eneo moja kwenda jingine;
(i) kuhamasisha wafugaji kuvuna mifugo yao mara kwa mara ili kuwa na idadi ya mifugo yenye kuleta tija;
(j) kuandaa operesheni za kubaini mifugo iliyoingizwa bila kibali wala utaratibu ulioidhinishwa na Halmashauri; na
(k) kuhakikisha kwamba mfugaji anafuga kwa kuzingatia kibali kilichotolewa.

Wajibu wa mfugaji

**5**.-(1) Kila mfugaji atakuwa na wajibu wa kuzingatia masharti ya ufugaji yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi atahakikisha kuwa-
(a) anafuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(b) anazingatia maelekezo yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, ikiwa anafanya ufugaji wa ndani;
(c) mifugo inapata malisho, chakula na maji kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;
(d) anahudhuria mafunzo ya ufugaji bora;
(e) anadhibiti magonjwa ya wanyama kwa kuogesha mifugo na kuipa chanjo;

(f) mifugo inawekewa alama maalumu kwa ajili ya utambuzi bila kuathiri ubora na thamani ya ngozi;
(g) anakuwa na kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(h) ana kibali cha kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo;
(i) anauza mifugo katika masoko na minada iliyoidhinishwa au eneo lingine kwa taarifa maalum;
(j) atahakikisha anafuga idadi ya mifugo ambayo haitasababisha usumbufu kwa wadau wa kilimo kama ilivyoidhinishwa kwenye kibali cha Halmashauri;
(k) atalazimika kutoa taarifa yoyote juu ya kutokea kwa magonjwa ya mifugo akiyaona au kuhisi au kuyatambua dhidi ya mifugo yake; na
(l) ataheshimu masharti ya karantini wakati wa magonjwa ya mlipuko.

Kibali cha kufuga wanyama

**6**.-(1) Mtu yeyote atakayekusudia kufuga mifugo atapaswa kuomba kibali cha kufuga kutoka kwa Halmashauri.

(2) Kibali cha ufugaji hakitakuwa na gharama na kitakuwa cha miaka mitatu kuanzia tarehe kilipotolewa na kinaweza kuhuishwa.

(3) Kibali cha ufugaji kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(4) Halmashauri inaweza kufuta kibali cha mtu yeyote atakayekiuka taratibu za ufugaji zilizoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mfugaji

**7**. Mfugaji hataruhusiwa-
(a) kufuga bila kibali kutoka Halmashauri;
(b) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;
(c) kufuga mifugo zaidi ya idadi inayoruhusiwa na Halmashaur;
(d) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(e) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(f) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali; na
(g) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa bila kibali maalum cha Halmashauri.

Kibali cha kusafirisha mifugo

**8**.-(1) Mtu anayekusudia kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo ikiwa mfugaji au msafirishaji atatoa uthibitisho wa umiliki wa mifugo kwa Afisa Mwidhiniwa.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukamata mifugo na kutoza faini kwa mmiliki wa mifugo inayosafirishwa kinyume na Sheria Ndogo hizi.

Kudhibiti mifugo inayozurura

**9**.-(1) Kila mfugaji atakuwa na wajibu wa kuzuia au kudhibiti mifugo kuzurura nje ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji.

(2) Kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi ulioandaliwa, Halmashauri itadhibiti mifugo inayozurura katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa matumizi hayo.

(3) Endapo mifugo itakamatwa ikiwa inazurura, mfugaji atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu kumi kwa kila siku kwa kila mfugo.

(4) Endapo mifugo iliyokamatwa haitachukuliwa na mfugaji ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya mahakama, na fedha zitakazopatikana zitawasilishwa kwa mmliki wa mifugo mara baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mifugo, gharama ya mahakama na gharama ya mnada.

(5) Kabla ya kuuza mifugo kwa mnada, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku zisizozidi saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mifugo hiyo na endapo kama mifugo itauzwa na mmiliki hataonekana ndani ya muda wa siku ishirini na nane tangu tarehe ya mnada, fedha hizo zitahesabika kama mapato ya Halmashauri.

(6) Endapo mifugo itakufa kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama isipokuwa kama kifo kimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na mazao ya mifugo

**10**.-(1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kukagua mifugo au mazao ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na anaweza kukataa aina yoyote ya mifugo au mazao ya mifugo kuingizwa au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba mifugo au mazao ya mifugo yanaweza kuhatarisha afya au usalama wa watumiaji au mifugo mingine.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kufanya ukaguzi muda wowote ndani ya masaa ishirini na nne (24) kwa lengo la utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(3) Mtu atakaye mzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa anatenda kosa.

Taratibu za biashara ya mifugo na mazao ya mifugo

**11**.-(1) Kabla ya kuanza biashara ya mifugo na mazao ya mifugo mfanyabiashara atapaswa kuwa na leseni, baua ya utambulisho kutoka serikali ya mtaa au Kijiji anachotoka na vibali kutoka mamlaka husika vinavyohusu kuuza na kununua mifugo na mazao ya mifugo na atatakiwa kuwasilisha vibali vyake Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mfanyabiashara wa mifugo inayopelekwa au kutolewa mnadani au machinjioni atatakiwa kuwa na kibali maalum kutoka Halmashauri.

(3) Mfanyabiashara anayeingiza mifugo ndani ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(4) Mfanyabiashara wa mifugo atatakiwa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

(5) Mtu yeyote atapaswa kuuza au kununua mifugo katika minada na masoko yanayotambulika kwa mujibu wa sheria.

(6) Mtu atakayekamatwa akisafirisha mifugo bila kibali au kuuza mifugo katika eneo ambalo halijaidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo, atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini kwa kila mfugo.

(7) Minada ya mifugo au magulio ya mifugo yatafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kwenye maeneo yaliyoruhusiwa.

Kuingiza wanyama katika machinjio

**12**.-(1) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kuhakikisha umiliki wa mnyama anayekusudiwa kuchinjwa unathibitishwa kabla ya kuingizwa katika eneo la machinjio.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakagua kibali cha usafirishaji wa mifugo na nyaraka nyingine zinazothibitisha umiliki.

(3) Meneja wa machinjio atatunza rejesta ya wanyama waliopokelewa machinjioni ambayo itaainisha aina ya mnyama, jinsi, umri na taarifa za mmiliki.

Taratibu za kuingia machinjioni

**13.** Mtu yeyote anayetaka kuingia katika eneo la machinjio anatakiwa kuomba kibali kwa maandishi kabla ya siku ya kutembelea na meneja wa machinjio anaweza kumruhusu mtu huyo na kumtaka kuvaa mavazi maalumu yanayopatikana katika eneo la machinjio.

Ukaguzi wa wanyama

**14**.-(1) Mifugo inayokusudiwa kuchinjwa katika machinjio itafanyiwa ukaguzi wa awali na mkaguzi wa nyama kabla ya kuchinjwa.

(2) Endapo baada ya ukaguzi mifugo itagundulika kuwa na magonjwa hatarishi kwa afya ya binadamu au

haijachanjwa, mifugo hiyo itahifadhiwa katika eneo maalumu kwa ajili ya matibabu.

Sura ya 156

(3) Kabla ya mifugo kutengwa, taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya magonjwa ya wanyama zitafuatwa.

(4) Endapo mifugo iliyotengwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) itaendelea kuwa na maradhi, Afisa Mwidhiniwa atamtaka mmiliki wa mifugo kuiondoa nje ya eneo la machinjio kwa matibabu zaidi.

(5) Endapo mmiliki atashindwa kuondoa mifugo iliyotengwa ndani ya muda wa saa kumi na mbili tangu amri ya kuondolewa kwa mifugo itolewe, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuamuru mifugo hiyo kuteketezwa kwa gharama ya mmiliki.

(6) Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuchukua kumbukumbu za mmiliki na mifugo iliyobainika kuwa na magonjwa na kuiweka alama maalumu ya utambuzi.

Udhibiti wa shughuli za machinjio

**15**.-(1) Meneja au mmiliki wa machinjio atahakikisha kuwa shughuli za machinjio zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za afya ikiwa ni pamoja na -

(a) watoa huduma kupima afya kila baada ya miezi sita;
(b) watoa huduma kuwa wasafi na kuvaa mavazi maalumu kwa ajili ya kazi hiyo;
(c) kutoruhusu mkusanyiko isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri;
(d) kutoruhusu kufanyika biashara nyingine yoyote katika eneo la machinjio.

(2) Mtu hataruhusiwa kuweka bucha, duka la nyama au biashara yoyote ya nyama ndani ya mita mia mbili kutoka eneo la machinjio.

(3) Mtu hataruhusiwa kuchinja mifugo bila mifugo hiyo kufanyiwa ukaguzi.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mtu kuchinja mifugo mahali pengine ambapo si machinjio kwa madhumuni ya kuuza isipokuwa mara baada ya kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa.

(5) Mtu hataruhusiwa kuingiza mifugo katika machinjio kwa ajili ya kuchinja baada ya saa kumi na moja kamili jioni isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(6) Mtu hataruhusiwa kutoa nje ya eneo la machinjio mnyama aliye hai au aliyekufa au nyama bila ya idhini ya maandishi ya meneja wa machinjio.

(7) Mtu mwenye majeraha, michubuko au ugonjwa unaoambukiza kwa kugusana au kwa njia ya hewa hataruhusiwa kuingia katika eneo la machinjio.

Ukaguzi wa nyama

**16**.-(1) Mkaguzi wa nyama atakuwa na wajibu wa kukagua nyama katika eno la machinjio baada ya mifugo kuchinjwa kwa ajili ya kubaini ubora wa nyama kwa matumizi ya binadamu.

(2) Endapo itabainika kuwa nyama iliyokaguliwa-

(a) inafaa kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi wa nyama atagonga nyama hiyo muhuri unaothibitisha kuwa nyama iliyokaguliwa ni salama kwa matumizi ya binadamu; au

(b) haifai kwa matumizi ya binadamu, nyama hiyo itateketezwa kwa kuchomwa moto au kwa njia nyingine itakayoonekana inafaa na mkaguzi wa nyama atachukua kumbukumbu za nyama hiyo na za mmiliki wake.

(3) Endapo matokeo ya vipimo vya awali yatakuwa na mashaka kuhusu ubora wa nyama kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi wa nyama atahakikisha kuwa nyama husika inahifadhiwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne ili kuruhusu vipimo zaidi vya kimaabara kufanyika.

(4) Meneja au mmiliki wa machinjio atatunza rejesta ya nyama zilizokaguliwa ambayo itaonesha aina ya nyama, jinsi, umri, uzito na taarifa za mmiliki na kama nyama inafaa au haifai kwa matumizi ya binadamu.

Rejesta ya wanyama

**17**. Meneja au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kutunza rejesta ya wanyama waliochinjwa na ambao hawajachinjwa ikionesha aina, jinsi, umri, uzito wa mnyama, na jina na anwani ya mmiliki wa mnyama.

Wajibu wa mfanyabiashara wa bucha na maduka ya nyama

**18**. Kila mfanyabiashara wa bucha au duka la nyama atahakikisha-

(a) ana leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;
(b) katika duka lake kuna kabati la vioo la kuzuia inzi na wadudu wengine wataambao, jokofu la kuhifadhia nyama na pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(c) jengo lake la biashara lina mwanga wa kutosha, umeme, maji safi na salama na vifaa maalumu vya kupima na kukatia nyama;
(d) nyama imekaguliwa na kugongwa muhuri na mkaguzi aliyeidhinishwa;
(e) muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote ambazo ni mabuti, koti na kofia;
(f) muuzaji anapima afya yake kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji;
(g) anatoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wowote wa ukaguzi; na
(h) biashara ya nyama inafanyika katika bucha na maduka maalumu.

Usafirishaji wa nyama

**19**.-(1) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalumu na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoainishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki au dereva wa gari la kubeba nyama atahakikisha kuwa gari-

(a) limesajiliwa Halmashauri kwa ajili ya kubeba nyama;
(b) limetambuliwa na Halmashauri na kupewa namba ya utambuzi;
(c) linakaguliwa na Halmashauri kila baada ya miezi mitatu na kupewa cheti cha ukaguzi;
(d) lina sanduku la aluminiamu lenye mfuniko na limepakwa rangi nyeupe, mstari mwekundu na namba ya utambuzi; na
(e) halibebi kitu kingine tofauti na nyama.

Udhibiti wa ufugaji wa mbwa

**20**.-(1) Mtu anayefuga au anayekusudia kufuga mbwa atapaswa kutoa taarifa kwa Halmashauri kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya umiliki wa mbwa huyo.

(2) Mfugaji wa mbwa atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuhakikisha mbwa anayemfuga anapata chanjo na analipa ada ya chanjo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;

(b) kuonesha cheti cha chanjo ya mbwa kabla ya kupata au kuhuisha kibali kilichoisha muda wake;

(c) kumfungia mbwa wake wakati wote wa mchana na anaweza kumfungulia kuanzia saa nne kamili usiku na kumfungia saa kumi na moja alfajiri;

(d) kuogesha mbwa kila baada ya siku saba ili kudhibiti magonjwa na wadudu wasumbufu;

(e) kumfunga mbwa kwa mnyororo maalumu wakati wa kutembea naye kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa mujibu wa sheria; na

(f) endapo anakusudia kusafirisha mbwa, atalazimika kuwa na kasha maalumu.

Makosa na adhabu

**21**. Mtu anatenda kosa iwapo-

(a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mifugo yake ili kuzuia magonjwa;

(b) atalisha au kunywesha mfugo au mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) atashindwa au kwa makusudi hatatoa taarifa juu ya uwepo wa au dalili za ugonjwa au kifo cha ghafla cha mfugo au mifugo katika banda lake;

(d) atauza na kufuga mifugo eneo ambalo halijaruhusiwa;

(e) ataruhusu mifugo kuzurura;

(f) atakataa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mifugo;

(g) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa, mkaguzi wa nyama, meneja au mmiliki wa

machinjio kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi; au

(h) ataingiza mifugo kutoka nje ya Halmashauri bila ya kibali.

(i) atashawishi au kusababisha mtu mwingine kutotekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi; au

(j) atakiuka masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya kanuni ndogo ya (1) atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita jela na kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

Kufililisha kosa

**22**. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2)(b))*

MAELEKEZO KUHUSU UFUGAJI WA NDANI

| Namba | Aina ya mifugo | Idadi | Maelekezo |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |
| 4. | | | |
| 5. | | | |

**Maelekezo yajikite kueleza aina ya mifugo, idadi kulingana na ukubwa wa eneo, mila na desturi za wakazi wa eneo husika kwa kuzingatia adha inayoweza kusababishwa na ufugaji katika eneo husika**

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya* 6(3)*)*

KIBALI CHA KUFUGA MIFUGO

Jina……………………………………………………………………......................................

Anuani………………………………………………………………………………………

Ameruhusiwa kufuga wanyama wafuatao katika eneo la ………………………………………

| Na | Aina ya Mnyama | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ng`ombe | |
| 2 | Mbuzi | |
| 3 | Kondoo | |
| 4 | Nguruwe | |
| 5 | Ngamia | |
| 6 | Punda | |
| 7 | Paka | |
| 8 | Farasi | |
| 9 | Sungura | |
| 10 | Mbwa | |
| 11 | Kuku/Bata | |
| 12 | Wanyama wengine (Wataje) | |

Kibali kitakuwa kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kwa Wanyama wa mapambo (petty animals) kuanzia tarehe ………………………… hadi tarehe ………………………………

Kimetolewa na :

Jina la Afisa Mwidhiniwa ………………………………………

Saini …………………………………………………………….

Cheo …………………………………………………………….

Tarehe …………………………………………………………..

Muhuri

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 8(1))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO

Jina ………………………………………………………………………………

Anuani ………………………………………………………………………..

Ameruhusiwa kusafirisha Wanyama wafuatao kutoka……………………….. kupitia njia za ……………………………………………….hadi …………………………………………

| Na | Aina ya Mnyama | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ng`ombe | |
| 2 | Mbuzi | |
| 3 | Kondoo | |
| 4 | Nguruwe | |
| 5 | Ngamia | |
| 6 | Punda | |
| 7 | Paka | |
| 8 | Farasi | |
| 9 | Sungura | |
| 10 | Mbwa | |
| 11 | Wanyama wengine (Wataje) | |

Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku ……kuanzia tarehe …………hadi tarehe ……………

Barua toka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/ Afisa Mifugo Kata inayothibitisha uhalali wa kumiliki mifugo/Wanyama hao imeambatanishwa.

Kimetolewa na:-

Jina la Afisa Mwidhiniwa ………………………………………………………………

Saini ……………………………………………………………………

Cheo …………………………………………………………………….

Tarehe …………………………………………………………………

Muhuri

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 22)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi……………………………………………………NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya .…… ya Sheria Ndogo za Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa za Mwaka, 2025.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, NAKUBALI kulipa faini ya shilingi ......................na ada ya shilingi................

NATHIBITISHA KWAMBA maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa mimi mwenyewe kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu

Leo hii tarehe………….ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina………………………………..Saini………………………

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:…………………......................................

Saini:…………………..….............................

Tarehe:..............................................................

Lakiri ya halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio la mkutano wa Baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya ruangwa uliofanyika tarehe 12-12-2023 na kushuhudiwa lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

FRANK FABIAN CHONYWA,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Ruangwa*

ANDREW CHRISTOPHER CHIKONGWE,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Ruangwa*

**NAKUBALI,**

**L.S**

Dodoma,
9 Aprili, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-Tamisemi*